KCPE 2003

KISWAHILI

SEHEMU YA KWANZA: LUGHA

Muda: Saa 1 dakika 40

For More Free KCPE Revision Past Papers and Answers
Visit http://www.freekcpepastpapers.com

JINSI YA KUJIBU MASWALI KWA MAKINI MAAGIZO YAFUATAYO

Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.

Ikiwa utataka kuandika chochote ambacho si jibu andika katika kijitabu hiki.

Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali.

JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU

Tumia penseli ya kawaida.

Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

NAMBA YAKO YA MTIHANI
JINA LAKO
JINA LA SHULE YAKO

. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.

. Usitie alama zozote nje ya visanduku.

. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.

). Kwa kila swali 1–50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.

). Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

Mfano:

Katika kijitabu cha maswali:

21. Kamilisha: Amani haiji .....

A. bila ncha ya upanga
B. ila kwa ncha ya upanga
C. kwenye ncha ya upanga
D. katika ncha ya upanga

Jibu sahihi ni B.

Katika karatasi ya majibu:

1	(A)	(B)	(C)	(D)	11	(A)	(B)	(C)	(D)	21	(A)	●	(C)	(D)	31	(A)	(B)	(C)	(D)	41	(A)	(B)	(C)	(D)

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **21**, kisanduku chenye herufi B ndicho kilichochorwa kistari.

. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.

. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

Tips on passing KCPE check @ http://www.freekcpepastpapers.com
Support through M-pesa 0720502479. This paper is not for resale.

Maswali 1 mpaka 15.

Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.

Tulikaa mkabala wa kidimbwi __1__ upepo na kutazama runinga. Kipindi tulichokitazama kilifanya nyoyo zetu kuatuka __2__ jitihada. Tuliona watoto wadogo ambao hali zao __3__. Vifupa vya mbavu __4__ viliweza kuhesabiwa na matumbo yao yalikuwa __5__ viriba. "Kwa nini watoto hawa kuwa hivi?" Baraza __6__. Maganga akajibu. "Watoto hawa wanaugua ugonjwa wa utapiamlo. Utapiamlo ni __7__ wa lishe bora mwilini. Tukila chakula __8__ mahitaji yetu ya mwili, tutashikwa na ugonjwa huu.

1.	A. tukifunga	B. tukipunguza	C. tukipunga	D. tukifungia
2.	A. na	B. kwa	C. katika	D. kwenye
3.	A. zilihuzunisha	B. zilihuzunika	C. zilihuzunishana	D. zilihuzunikia
4.	A. vyao	B. zao	C. lao	D. yao
5.	A. mithili za	B. mithili wa	C. mithili na	D. mithili ya
6.	A. alishauri	B. alijisaili	C. alisaili	D. alijiuliza
7.	A. upungufu	B. upunguzaji	C. kupunguza	D. kupungua
8.	A. kisichotoshana	B. kisichotosheka	C. kisichotoshewa	D. kisichotosheleza

Baada ya mtoto kuzaliwa, Mungu __9__ walimu wengi. Mwalimu wa kwanza wa mtoto ni mama. Yeye __10__ anayeanza kuujaza ukurasa __11__ wa ubongo wa mwanawe. Baba pia ana __12__ kubwa katika kumfunza na kumlea mtoto. Mazingira ya mtoto __13__ yeye huanza kuwa na walimu wengi wa __14__. Ikumbukwe kuwa __15__ mazingira anapokulia mtoto yatamfunza maadili yeye ataibuka kuwa mwadilifu.

9.	A. hutunukiwa	B. humtunukia	C. huwatunukia	D. anatunukiwa
10.	A. ndio	B. ndiwe	C. ndiyo	D. ndiye
11.	A. tupu	B. mtuvu	C. mtupu	D. tulivu
12.	A. madaraka	B. dhima	C. wajibu	D. wadhifa
13.	A. yanapopanuka	B. inapopanuka	C. zinapopanuka	D. anapopanuka
14.	A. kuigiwa	B. kuigana	C. kuigizana	D. kuiga
15.	A. hata kama	B. ijapokuwa	C. iwapo	D. ingawa

For More Free KCPE Revision Past Papers and Answers Visit http://www.freekcpepastpapers.com

Tips on passing KCPE check @ http://www.freekcpepastpapers.com
Support through M-pesa 0720502479. This paper is not for resale.

For More Free KCPE Revision Past Papers and Answers
Visit http://www.freekcpepastpapers.com

Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.

16. Chagua kivumishi katika sentensi ifuatayo
Mtoto mtiifu haonywi mara nyingi
A. haonywi
B. mtoto
C. mtiifu
D. mara nyingi

17. Ni msemo upi unaotoa maana ya: Kumpa mtu sifa asizostahili
A. Kumwonea mjicho
B. Kuuma ngoa
C. Kuinbwagia zani
D. Kumvika kilemba cha ukoka

18. Jengo la kuhifadhia nafaka huitwa
A. ngome
B. ghala
C. ufuo
D. maktaba

19. Chagua sentensi iliyo sahihi
A. Vikombe ambavyo vilinunuliwa ni visafi
B. Vikombe ambavyo vilivyonunuliwa ni visafi
C. Vikombe ambavyo vilinunuliwa ni safi
D. Vikombe ambavyo vilivyonunuliwa ni safi

20. Chagua sentensi iliyoakifishwa ipasavyo
A. Alitumwa kununua vitu vifuatavyo: sukari, vitunguu, mchele, na ngano
B. Alitumwa kununua vitu vifuatavyo, sukari, vitunguu, mchele na ngano.
C. Alitumwa kununua vitu vifuatavyo: sukari, vitunguu, mchele na ngano.
D. Alitumwa kununua vitu vifuatavyo, sukari, vitunguu, mchele, na ngano.

21. Ukubwa wa sentensi
Ndege mkubwa alipaa angani ni:
A. Ndege kubwa alipaa angani.
B. Dege kubwa lilipaa angani.
C. Dege kubwa alipaa angani.
D. Ndege kubwa lilipaa angani.

22. Kitenzi kinachoweza kuundwa kutokana na jina mshindani ni
A. shinda
B. mshinde
C. kishindo
D. shindano

23. Ni sentensi ipi kati ya hizi iliyo na kwa ya kuonyesha sababu?
A. Alitembea kwa maringo
B. Alilima kwa jembe
C. Alialikwa kwa mwalimu mkuu.
D. Aliadhibiwa kwa utundu wake

24. Juma aligawa robo ya muwa sawasawa kwa wanawe wawili. Kila mmoja alipata
A. sudusi
B. robo mbili
C. thumuni
D. nusu

25. Hili ni umbo gani?

A. Mraba
B. Mche
C. Pia
D. Mstatili

26. Mwana wa simba huitwa
A. mtoto simba
B. simba marara
C. kinengwe
D. shibli

27. **Mdomo** ni kwa **binadamu**, **kidona** ni kwa
A. ndege
B. ndovu
C. kombamwiko
D. samaki

28. Chagua kikundi cha wadudu
A. Mchwa, Nzige, Panzi, Mkizi
B. Nge, Tai, Mbu, Kiroboto
C. Shore, Njiwa, Mende, Konokono
D. Sisimizi, Chungu, Nzige, Kumbikumbi

29. Kanusha:
Ndege akijenga kiota huishi humo.
A. Ndege anapojenga kiota haishi humo
B. Ndege akijenga kiota hataishi humo
C. Ndege asipojenga kiota haishi humo
D. Ndege ajengapo kiota hataishi humo

30. Onyesha kielezi katika sentensi hii: Wazee wengi walitembea polepole
A. Wazee
B. Polepole
C. Walitembea
D. Wengi

Tips on passing KCPE check @ http://www.freekcpepastpapers.com
Support through M-pesa 0720502479. This paper is not for resale.

Soma kifungu kifuatacho, kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.

Bwana Limbuka alikuwa amekuzwa katika mazingira ya kazi nyingi. Wazazi wake waliamini kuwa, mtu akifunzwa kazi mapema, atakuwa mkakamavu maishani. Kwake Limbuka alichukulia kinyume. Kimoyomoyo, alijiapia kuwa akipata kazi ni ‘aoe, kisha apate watoto, hatawasumbua. Alitia bidii shuleni na akapita mitihani yake ya viwango vya juu. Baadaye, akabahatika kama mtende, akavuka mabonde na milima hadi huko ughaibuni kuongezea masomo.

Akiwa bado ana lile mulitiduku lake la hapo awali, aliziangalia familia za huko na kuvutiwa. Akathibitisha kuwa makazi ya kikwao ni ya kishamba. Akasahau kuwa, kisomo cha kiiadi alichopewa na wazazi kilikuwa ndicho chanzo cha ufanisi wake.

Baada ya miaka si haba alirudi kwao, akaoa na kujaliwa watoto wawili. Alimwapia mkewe kuwa, yeye hatathubutu kuchikicha makuzi ya kizamani. Hakujua kuwa mwacha mila ni mtumwa. Hapo basi wakawalea watoto kama mayai. Watoto walipoguswa kidogo, walishtakia hali kwa wavyele wao, nao waliwabwekea “wachokozi” kwa hasira. Watu wakabakia macho tu! Wakamngojea “msema kweli wa maisha”. Watoto wakaota pembe za kinyati. Kwa kukosa kazi yoyote, waliigiza lolote lile waliloliona katika runinga. Walifokokwa ovyo popote pale bila ya tahayuri yoyote. Walipokua kidogo walianza kunywa pombe, kuvuta sigara na kutumia madawa ya kulevya.

Vituko vilipozidi na kuvuka mipaka, walianza kuwadharau na kuwaaibisha wageni maskini waliowatembelea huko kwao. Waliowahi kufika kwao kwa vigari vya supana mikononi walichekwa. Hawa watoto walishangaa walipoona watu wakipanda “matatu” au “mabasi”. Walipokwenda kuchukuliwa shuleni kwa gari walilolipuuza, walijificha na kusema, “Hilo ni gari la sokoni, halitufai”. Walipoingia kwenye maduka, walichagua bidhaa za bei ghali. Bwana Limbuka na mkewe waliridhi matakwa ya watoto wao wakidhani kuwa huko ndiko kupenda. Walisahau kuwa kuna leo na kesho. Wakasikika wakisema, “Watoto safi sana hawa. Ni jasiri na werevu. Hawana undani wowote.” Hawakukumbuka kuwa kuna yale yanayofaa kusemwa na kuna yale ya kunezea. Maneno mengine huchoma watu nyoyoni.

Watoto wa Limbuka walizidi kudidimia kisimani. Shule nayo ikawapiga chenga. Wakashindwa mitihani yao ya kidato cha nne. Katika hali ya kuokoa jahazi lililokuwa likizama, wazazi wakawapa mitaji ya kuanzishia biashara. Baada ya muda mfupi mambo yalivurugika. Mali yote ikafujwa kwa kasi kwani buyu la asali halichovwi mara moja. Mwishowe ukata uliwanyemelea wakawa maskini hohehahe wasioweza hata kuwasaidia wazazi wao wazee. Walibaki kuwayawaya mitaani na kuzubaliwa na walimwengu. Limbuka na mkewe nao walijifunza kuwa mtoto hakuzwi kwa kubwagiwa mapesa na kuengwaengwa. Anafaa kufunzwa jinsi ya kuukabili ulimwengu bila ya kutegemea nundu za wazazi. Mtegemea cha ndugu hufa maskini.

For More Free KCPE Revision Past Papers and Answers
Visit http://www.freekcpepastpapers.com

Tips on passing KCPE check @ http://www.freekcpepastpapers.com
Support through M-pesa 0720502479. This paper is not for resale.

For More Free KCPE Revision Past Papers and Answers
Visit http://www.freekcpepastpapers.com

31. Wazazi wa Limbuka
A. waliuwahi udongo ungali maji
B. hawakujali maslahi ya mwana wao
C. walimpa Limbuka fursa ya kujiamulia
D. walikuwa watesi na wasumbufu

32. Limbuka alianza kuwa tu anazamo tofauti na makuzi yake
A. wakati alioa
B. alipopata watoto
C. alipokuwa akikingezea masomo
D. akiwa kyungibani kwa wazazi wake

33. Maana ya "kwake Limbuka alichukulia kinyume" ni kusema:
A. Kufunzwa kazi mapema kunasaidia mtu na familia yake
B. Kufunzwa kazi nyingi ni msingi wa bidii maishani
C. Kufunzwa kazi mapema hakuleti faida yoyote maishani
D. Kufunzwa kazi mapema ni kinyume cha sheria

34. Ni mambo gani yanayoonyesha kuwa Limbuka ni mwacha mila?
A. Kutopenda kazi nyingi, kwenda ng'ambo na kuvutiwa na makuzi ya kigeni.
B. Kuvutiwa na familia za ng'ambo, kupuuza makuzi ya jadi na kuwaonea watoto fahari hata wakiropokwa.
C. Kutowakaripia watoto, kuwanunulia bidhaa ghali na kuwaonea fahari.
D. Kuwaonea watoto fahari hata wakiropokwa, kuwapa mitaji na kupuuza malezi ya jadi.

35. Ni zipi kati ya hizi <u>hazikuwa</u> tabia za watoto wa Limbuka?
A. Kuwaauni wazazi na kutia bidii shuleni.
B. Kulewa na kudharau watu.
C. Kuvuta sigara, kuropokwa na kupenda makuu.
D. Kuiga, kutojali hisia za watu na kuwaaibisha.

36. <u>Walipokwenda kuchukuliwa shuleni kwa gari</u> walilolipuuza, <u>walijificha na kusema, "Hilo ni gari la sokoni, lalitufai"</u>. Hali hii inamaanisha kuwa
A. wenzao shuleni walikuwa na magari bora zaidi
B. hawakupenda kwenda sokoni kwa gari lisilofaa
C. hawakupenda vigari vya supana mikononi
D. nyumbani kulikuwa na gari bora kuliko hilo

37. "Mchelea mwana kulia, hulia yeye." Limbuka na mkewe walilia kwa:
A. kuwapatia watoto wao mitaji na mali
B. kutolinda watoto wao wakati wakiwa wazee
C. kukosa mtu wa kuwasaidia wakiwa wazee
D. kusumbuliwa na ukosefu wa mali nyingi.

38. Maana ya <u>kuukabili ulimwengu bila ya kutegemea nundu</u> ni
A. mtu kuweza kujikimu bila ya kutarajia misaada
B. kuuingilia ulimwengu kwa kushauriwa na wazazi
C. kuuingilia ulimwengu bila kujali matokeo
D. mtu kupambana na maisha kwa kutegemea wengine

39. Msimamo wa mwandishi ni kuwa
A. makuzi ya kigeni ni bora kuliko ya kijadi
B. watoto wakilelewa bila kufunzwa maadili hupotoka
C. watoto wakipata elimu ya juu huharibika
D. watoto wanapopotoka wapewe mitaji na mali

40. <u>Ughaibuni</u> ni
A. nchi za uzunguni
B. nchi za masomo ya juu
C. nchi zilizoendelea
D. nchi za mbali

Tips on passing KCPE check @ http://www.freekcpepastpapers.com
Support through M-pesa 0720502479. This paper is not for resale.

Soma kifungu hiki kisha ujibu maswali 41–50.

Masikio ni sehemu muhimu sana ya mwili. Viumbe wengi wamepewa masikio mawili ya kunasia habari. Masikio hutakiwa kusafishwa vizuri wakati wowote mtu anapooga au kunawa. Nta za masikioni hufaa kuondolewa kwa uangalifu. Baadhi ya watu huyaharibu masikio kwa kuyachokorachokora kwa njiti za viberiti. Badala ya kuutoa uchafu huo kwa uzuri, wanaukandamizia ndani ya sikio. Wengine huingiza vitu vingine visivyofaa wanapopatwa na mwasho masikioni. Je, umewahi kufikiria jinsi kidubwasha kilichotokomezwa na kudidimia sikioni, kinavyoweza kuguguna na viungo vingine na kusababisha taabu kubwa? Idhihirike kuwa, kuingiza vijidude kama hivyo masikioni kutasababisha kuziba kwa masikio. Kuzibuliwa kwa masikio hayo huweza kugeuka kuwa ngoma ya kuya na kusababisha uziwi. Uziwi wa kujitakia ni kama mtu kujipalia makaa.

Baadhi ya masikio huharibiwa na sauti kubwa kama ya muziki. Redio na televisheni zinafaa kufunguliwa sauti za wastani. Sauti kubwa za kushtua moyo hazidhuru tu masikio, bali huweza kuleta maafa kwa wale wagonjwa wenye maradhi ya moyo. Ni vyema kuyajali maslahi ya wenzetu. Baadhi ya vijana huonea fahari hali hiyo ya kuwandisha sana sauti za redio majumbani au kwenye "matatu". Tabia hiyo hukera na huwadhuru hata wahusika wenyewe bila kujua. Isitoshe, hali hii huweza kuleta mfarakano kwa majirani. Uangushaji wa vyombo kama sahani na vyuma sakafuni pia huathiri. Kelele zinazofanywa darasani au mikutanoni nazo hazifai. Kulitesatesa sikio kwa kulitogatoga kila mahali pia huleta maumivu. Kutumia herini masikioni mwa madini hafifu yasiyopatana na ngozi ya mtu binafsi huleta usumbufu mkubwa. Wakati nywele zinapooshwa na kemikali kuachwa kuingia masikioni, huwa ni hatari. Kadhalika, watoto wadogo wanapocheza huweza kujiingiza nafaka masikioni au kujidunga kwa vitu vyenye ncha kali. Uvutaji wa masikio kama adhabu ni tabia isiyofaa kwani huhasiri masikio.

Ni vyema mtu akiwa na shida amuone daktari ama sivyo madhara makubwa yatazuka. Wakati masikio yanapoanza kutoa usaha yatibiwe mara moja. Kutokwa kwa usaha ni dalili ya kuwa na kidonda kisichofaa kutafutiwa dawa za kiholela. Wataalamu wa masikio ndio tu wanaofaa kuhusishwa na matibabu hayo.

For More Free KCPE Revision Past Papers and Answers
Visit http://www.freekcpepastpapers.com
Tips on passing KCPE check @ http://www.freekcpepastpapers.com
Support through M-pesa 0720502479. This paper is not for resale.

For More Free KCPE Revision Past Papers and Answers
Visit http://www.freekcpepastpapers.com

1. Masikio ni sehemu ya
   A. kiwiliwili
   B. ndewe
   C. kichwa
   D. shavu

2. Uchafu hukandamizwa masikioni kwa
   A. kutotolewa kwa njia inayofaa
   B. kuziba kwa masikio
   C. kuingiza vitu visivyofaa
   D. kuwa na kidonda sikioni

43. Ni hali gani inayotanya watu kuchokorachokora masikio?
   A. yanapovimba
   B. yanapotoa usaha
   C. yanapovimba
   D. yanapowasha

44. Sauti kubwa za kushtua
   A. zinasababisha ugonjwa wa moyo
   B. zinaweza kudhuru wagonjwa wa moyo
   C. hazitolewi palipo na wagonjwa wa moyo
   D. zinadhuru tu wagonjwa wa moyo

45. Ni mambo gani yanayofaa kuepukwa majumbani ili kuzuia watu wasiharibike masikio?
   A. Kupandisha sauti kwenye matatu na kuingiza vitu masikioni.
   B. Kutoga masikio, kuweka kemikali na kumwona daktari.
   C. Kuangusha vyombo, kupiga kelele na kuvuta masikio.
   D. Kuongeza sauti, kutotoga masikio na kutovuta masikio.

46. Kwa nini tabia ya kupandisha sauti za redio majumbani huweza kuleta uhasama kwa majirani?
   A. Majirani huenda hawapendi kupigiwa kelele.
   B. Kwa sababu majirani hawana redio zao.
   C. Majirani wana ugonjwa wa masikio na moyo.
   D. Ni kawaida ya majirani kupenda uhasama.

47. Maana ya kidonda kisichofaa kutafutiwa dawa za kiholela ni
   A. kidonda kinachohitaji dawa za kiasili
   B. kidonda kisichoweza kupona kamwe
   C. kidonda kinachohitaji matibabu ya haraka zaidi
   D. kidonda kinachohitaji matibabu yenye uangalifu zaidi

48. Kujipalia makaa ni
   A. kujisababishia jambo
   B. kujiletea madhara
   C. kujiwekea mikaa
   D. kujiletea jambo

49. Chagua methali mwafaka inayoweza kutamika kueleza kifungu hiki
   A. Kipendacho moyo ... dawa
   B. Heri kufa jicho kuliko kufa moyo
   C. Usipoziba ufa utajenga ukuta
   D. Sikio la kufa halisikii dawa.

50. Fundisho la habari hii ni
   A. Kutunza masikio
   B. Kumwona daktari
   C. Kutocheza na vitu masikioni
   D. Kutopandisha sauti za redio

Tips on passing KCPE check @ http://www.freekcpepastpapers.com
Support through M-pesa 0720502479. This paper is not for resale.